

ATHARI ZA KANGA KWA UTAMADUNI WA MSWAHILI

Amina Ali Khamis

Mwalimu wa Skuli ya Sekondari ya Faraja

amralikh@gmail.com

0778859703

Na

Gora Akida Haji

Mwalimu wa Skuli ya Sekondari ya Faraja

hajigora82@gmail.com

0773127095

IKISIRI

Tamaduni za waswahili zimejikita katika lugha, mavazi, vyakula, taratibu za ndoa na mazishi (sherehe na misiba). Tamaduni hizi zimekuwa ni msingi wa utambulisho kwa jamii ya Waswahili. Kanga ni miongoni mwa vazi la Mswahili na limekuwa na dhima kubwa katika kutekeleza majukumu ya kiutamaduni. Vazi hili limekuwa ni kielelezo tosha cha usawiri wa matukio ya kijamii kutokana na matumizi ya lugha, maua na rangi za kanga. Uvaaji wa kanga huzingatia rangi, maua na semi kwa kuangalia muktadha halisi wa mvaaji wa kanga hizo. Kanga zinazovaliwa msibani, ni tofauti kabisa na kanga zinazovaliwa harusini kwa semi, maua na hata rangi yake. Vyote hivyo hujenga taswira halisi ya mvaaji, kwa kufikiria lengo la uvaaji wa vazi hilo. Waswahili hawatumii Kanga kama ni vazi la kujistiri tu, bali hutumia kama ni sehemu ya kuenzi mila na utamaduni wa jamii hiyo. Pia, kanga hutumika kama ni sehemu ya fasihi simulizi kwa lengo la kuburudisha nyoyo za wavaaji na wawaliwaji na kutoa ujumbe uliokusudiwa na mvaaji huyo. Fasihi inayowasilishwa katika muktadha huu ni fasihi yenye maana pana na yenye kina kirefu na uhalisi zaidi, kutokana na kuwa ni fasihi ya maneno na vitendo. Hivyo, makala hii ina kusudia kuchambua athari za uvaaji wa kanga kulingana na muktadha, majina ya kanga na semi zilizomo katika kanga kwa jamii ya Waswahili wa Zanzibar.